SURA YA KUMI

NAFASI YA TASFIDA NA MIIKO KATIKA MABADILIKO YA KISEMANTIKI YA MANENO YA KISWAHILI

Tirus Mutwiri Gichuru, Mosol Kandagor na *Sarah Ngesu*

Ikisiri

Wanajamii hujaribu iwezekanavyo kuepuka lugha-mwiko inayoibua fedheha, maudhi au kuvunja kaida zilizopo kwa kutumia lugha yenye heshima na staha. Makala haya yamejadili nafasi ya tasfida na miiko katika mchakato wa mabadiliko ya maana za maneno ya Kiswahili kwa kuchanganua mifano mahususi. Asili ya data iliyochanganuliwa katika makala haya ni kutoka kwa matini teule za kabla ya Karne ya Ishirini na kutoka katika kamusi za Kiswahili sanifu za karne ya Ishirini na moja. Uchanganuzi umebainisha kuwa tasfida na miiko zimechangia pakubwa kuleta mabadiliko ya maana za maneno ya Kiswahili kwa kuwa huchukua maneno yaliyopo katika lugha na kuyatwika maana mpya kwa madhumuni ya kusitiri hisia hasi. Kadhalika, miiko huambukiza maneno mengine umatusiumatusi; hali ambayo hufanya wanajamii kubuni msururu wa maneno yanayoambatana na maneno husika. Hali hii hupanua msamiati wa Kiswahili.

***Maneno Muhimu**: Mabadiliko ya Kisemantiki, Maneno-Mwiko, Mwiiko, Tasfida*

Utangulizi

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Gichuru (2020), ulibaini kuwa maswala ya kisaikolojia yanayoambatana na miiko na tasfida yanachangia pakubwa katika maendeleo na mabadiliko ya maana za maneno ya Kiswahili. Maswala yanayohusiana na imani, itikadi, kaida, tajriba na falsafa ya wanajamii yanajenga sehemu muhimu ya utambuzi inayomsaidia binadamu kuufasiri ulimwengu wake halisi na wa kidhahania; yakiwapo maumbo mbalimbali ya lugha (Gichuru, 2020). Katika utafiti husika, sampuli ya maneno mia mbili ilichanganuliwa ili kubainisha mbinu za kisemantiki zilizohusika katika kuleta mageuko ya maana. Japo mbinu ya tasfida ilichangia asilimia sita tu ya mabadiliko yaliyobainika, kunayo masuala ya kipekee yaliyodhihirika katika mfanyiko huu. Ilibainika kuwa mbinu ya tasfida ilijikita katika vikoa maana maalumu kinyume na mbinu nyinginezo zilizoonekana kusambaa katika makumbo yote yaliyoshirikishwa. Mathalani, asilimia 83% ya maneno ya vitu vitokavyo katika mwili yanatumia lugha ya kitasfida. Nayo maneno-mwiko yalionekana kujibaniza katika makumbo machache. Upekee huu wa tasfida na lugha mwiko ndio umechochea uandishi wa makala hii.

Mwanadamu ana uwezo wa kuhamisha dhana baina ya mawanda ya kiutambuzi kupitia lugha ya kitamathali hususan sitiari na metonimu (Lakoff & Mark 1980). Uwezo huu pia husaidia kukabiliana na dhana zenye umatusi na miiko kupitia matumizi ya kauli za kitasfida. Uwezo wa mwanadamu wa kuunda maneno na kauli za kitasfida ni njia mojawapo ya kukabiliana na lugha mwiko na njia ya kudhibiti mabadiliko yanayotokana na maendeleo ya jamii. Ni muhimu nifafanue kwa ufupi dhana za tasfida na miiko.

Dhana ya Tasfida na Miiko

Tasfida ni *lugha ya staha au ya kificho badala ya kutumia moja kwa moja lugha ya matusi au yenye kukera ikitumiwa hadharani* (BAKITA 2015). Hii ni lugha inayozingatia heshima na kufunika aibu fulani kutegemea miiko, tamaduni, tajriba na vikwazo vya kijamii. Ni neno au kauli inayowakilisha mwiko (Fromkin, Rodman na Hyams 2011). Mwiko (*miiko*, wingi) ni jambo lililokatazwa katika jamii na watu wa jamii hiyo. Madhara yanayotokana na matumizi ya maneno-mwiko hukitwa katika imani na falsafa ya wanajamii. Neno husemekana kuwa neno-mwiko ikiwa linaibua hisia mbaya zisizofurahisha wasikilizaji au linaaminika kuleta mikosi na bahati mbaya kwa wanajamii. Kwa mfano, Schadeberg (1991) anaeleza kuwa Wanyamwezi walikwepa kutaja neno *nshiimba* (simba) wakati wa usiku na badala yake kutumia *fahali*. Hapa neno *fahali* limetwikwa maana ya ziada. Anadokeza kuwa huenda neno 'simba' lilitumika awali kutajia wanyama ambao si wakali kama simba. Msimamo wa Schadeberg (ibid) unatokana na kupatikana kwa shina lili hili katika majina ya wanyama wengineo katika lugha kadhaa za Afrika Mashariki. Zingatia mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 1

Neno	*Lugha*	*Kiswahili*	*Kiingereza*
Shimba	Kigweno (Tanzania)	Chui	Leopard
Dhimba	Kikuyu (Kenya)	Nguchiro mweusi	Black mongoose
Kasimba	Kiganda (Uganda)	Kanu/kala	Genet
Nthimba	Kikamba (Kenya)	Paka mwitu	Wild cat
Shimba	Ki-Shambala (Tanzania)	Simba	Lion

Asili: Schadeberg (1991:110)

Wanyama waliotajwa katika jedwali 1 wanakaribiana kifamilia kwani wote ni wala-nyama. Pia, jamii ya Wameru ilikwepa kutaja majina mahususi ya *mbiti* (wanyama wala-watu) wakati wa usiku kwa imani kuwa watoto wangepata jinamizi mbaya wanapolala. Basi lugha-mwiko ni swala lenye uzito katika matumizi ya lugha katika jamii.

Maneno mpya ya kitasfida hubuniwa katika hali ya kuyaepuka maneno-mwiko au maneno yanayozua hisia zisizofaa (Gathiga 2010, Gachara 2012). Ni mbinu ya kupunguza makali ya lugha inayoambatana na lugha-mwiko. Zifuatazo ni baadhi ya sifa za tasfida na miiko kama zilivyodokezwa katika Allan & Burridge (1991) na Samoškaite (2011):

Sifa za tasfida

(i) Tasfida ni neno au kauli inayotumika badala ya neno au kauli iliyobeba maana hasi.

(ii) Huwa sinonimu ya neno au kauli iliyodhalilika na yenye umatusi umatusi.

(iii) Huwa kauli ya kujikinga na kukinga hadhira yako dhidi ya aibu na hisia zingine chukizi.

(iv) Hutumika kama njia ya upole, katika kundi lenye jinsia mbili kuzuia kuibua wazo kuwa mojawapo ya jinsia inadunishwa. Hudhibiti tabia ubabeume au uke.

(v) Huendelea kutumika katika jamii hadi pale 'zinapoambukizwa' hisia chukizi. Mara nyingi jamii hubuni misururu ya maneno ya kitasfida kuwakilisha dhana nyeti katika jamiii.

(vi) Kwa kiasi kikubwa hudhihirisha viwango vya elimu kwa watumizi wake. Waliosoma hutumia tasfida kwa wingi kuliko wasiosoma.

Nazo sifa za miiko ni zifuatazo:

Sifa za miiko

(i) Huwa maneno au kauli zinazowasilisha maana chukizi.

(ii) Hutaja dhana zinazofasiliwa na wanajamii kuwa za hatari na labda zinazosababisha kifo au magonjwa.

(iii) Huwa chanzo cha aibu na hufanya watu kuduwaa.

(iv) Huwa matokeo ya tabia zilizokatazwa katika miktadha mbalimbali ya jamii.

(v) Mara nyingine huwa ni maumbo ya kulaani au maapizo yanayozua migogoro ya kisaikolojia kwa wahusika.

(vi) Kinyume na tasfida, miiko huzusha hadhi ya dhana inayorejelewa.

(vii) Miiko hubadilika na wakati na muktadha hivi kwamba mwiko hutegemea jamii husika.

(viii) Maneno au kauli-mwiko hutumiwa zaidi na wanaume kuliko wanawake. Pia wasiosoma kuliko wasomi.

Ni bayana kuwa tasfida hutekeleza wajibu kinzani na miiko katika mfumo wa maana. Kwa kweli kuwapo kwa miiko katika jamii ndio sababu kuu ya kutumia lugha kitasfida. Maneno yanapotwikwa maana mpya za kitasfida hatimaye huzalisha maneno ya ziada yaliyo na maana zilizoimarika au zilizodhoofika. Maneno ya awali na yenye maana chanya huenda yakaendelea kutumika katika lugha au yakafifia kimatumizi. Kwa upande mwingine, maneno mwiko yanayoibua hisia hasi yanaweza kupoteza umatusiumatusi, yakaimarika na kuanza kutumika bila kuibua hisia zozote hasi katika mazungumzo ya kawaida.

Asili ya Data iliyochanganuliwa

Data iliyochanganuliwa katika makala haya ilikusanywa kutoka katika matini teule zinazosheheni Kiswahili kilichotumika katika ya Karne ya Ishirini na nyingine kukusanywa kutoka matini za Karne ya Ishirini na Ishirini na Moja. Matini zifuatazo ziliteuliwa: Krapf (1882) *Dictionary of Suaheli Language,* Steere. (1870): *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar. Revised Edition* by *Madan (1919),* Burt (1910) *Swahili Grammar and Vocabulary,* Abdulaziz (1979): *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry, na* Nabhany (2012): *Kandi ya*

Kiswahili. Matini nyingine ni kamusi mbalimbali za Kiswahili zilizoandikwa katika Karne ya Ishirini na Moja.

Uchanganuzi na Matokeo

Uchanganuzi ulihusisha maneno ambayo yamebadilika kisemantiki kupitia mbinu ya tasfida. Mbinu linganishi imetumika ambapo maana ya awali ya neno imelinganishwa na maana za kisasa. Kama ilivyoelezwa mwanzoni mwa makala, wanajamii hawapendi kutumia maneno-mwiko. Hali hii huwalazimu wanajamii kutumia maneno mengine kimafumbo ili kuepa hisia kali. Baadhi ya wasomaji wa makala haya huenda wakakumbana ana kwa ana na hali hiyo katika sehemu inayofuata ya uchanganuzi.

Ili kukidhi mahitaji ya makala hii na kuboresha uwasilivu, sampuli ya maneno arobaini ndiyo yamechanganuliwa katika makala haya. Maneno husika yamepangwa katika makundi saba kulingana na uhusiano wa kimaana. Zingatia mifano ifuatayo:

(i) Tasfida za Maungo ya Uzazi

Uchanganuzi umebainisha kuwa msamiati wa sehemu za uzazi umebadilika katika mapito ya wakati kukidhi kaida hizi za jamii. Hii hapa ni mifano:

i. *Kisimi, Uume, Uke, Mji, Shavu, Nyeti, Tupu*

Kisimi (Wingi, visimi) ni kinyama kinachofanana na kilimi kilichopo katikati ya mwanya wa uke au kuma ambacho huwa na mishipa ambayo humtia mwanamke hamu ya kushiriki ngono kikiguswa (Nabhany 2012). Pia huitwa *kinembe* (Kimvita), *mpeke* (Kibarawa), *kideme* (Kitukuu) na *msika* (Kisiu) kulingana na Kineene (2004). Neno hili linalohusisha mzizi **{–limi}** unaoambatana ulimi; *chochote kinachofanana na ulimi kiumbo* (TUKI 2013). Aidha, *kilimi* (udogo wa ulimi) hurejelea 'kipande kidogo cha nyama kilichoko ndani ya kinywa, chini ya shina la ulimi ambacho huwa na umbo linaloshabihiana na la ulimi, kidakatonge au kimio'. Kiungo *kisimi* kinashabihiana na kilimi kiumbo. Ni mwiko kukitaja hadharani katika jamii nyingi za Kiafrika hata wakiwamo Waswahili. Inaonekana matumizi ya /s/ badala ya /l/ ilikuwa mbinu ya kuongeza ubuye katika neno husika ili kupunguza makali na aibu linapotamkwa.

Maana msingi ya *uume* ni 'hali ya kuwa mwanamume'. Kimsingi, dhana ya 'uume' ni pana inayojumuisha umbo, kuwapo kwa viungo maalum, sauti na misuli yake miongoni mwa hulka zingine. Katika kisasa, neno hili hutumiwa kama tasfida kuwakilisha dhakari, jengelele au mboo. Hapa, dhana pana (uume) imetumiwa kuwakilisha dhana finyu (sehemu mahususi). Kadhalika, neno *uke* (hali ya kuwa mwanamke) hutumiwa katika kisasa kuwakilisha dhana finyu ya *kuma* au *doko*. Hali kadhalika, neno limebadilika ki-sitiari kuwakilisha 'tabia ya uoga'. Uoga huambatanishwa na wanawake katika baadhi ya jamii zenye taasubi ya kiume. Mabadiliko hayo yamewakilishwa katika mchoro ufuatao:

Kielelezo kuhusu mabadiliko ya Uke



Maana ina uzito kutoka katika kiini na uzito kufifia kutoka nje penye maana za kando kando. Neno lilibadilika kutokana na misukumo ya kitamaduni. Hali ya kizima kuwakilisha kisehemu chake huitwa metonimu.

Maana msingi ya *uchi* hali kutokuwa na nguo zozote za kusitiri mwili, kutokuwa na chochote. *Alipotoa nguo aliachwa ~*. Neno hili limetumiwa kama tasfida ya sehemu nzima ya uzazi. Matumizi ya aina hii ya kutaja sehemu pana na jumla kuwakilisha ndogo, hupunguza makali ya lugha. Kadhalika, kielezi cha mahali jumla *nyuma* hutumiwa kuwakilisha *mkundu* huku *mbele* ikiwakilisha *uume* na *uke*. Hata hivyo, matumizi haya hutegemea muktadha. Nayo maana msingi na ya awali ya *shavu* (tavu) ni 'sehemu iliyoko baina ya sikio na kidevu'. Kuna shavu ya kulia na ya kushoto. Katika kisasa ilihamishwa kisitiari na kuwa tasfida ya 'sehemu ya uke ambayo huwa pande mbili ya mwanya wa kuma, kulia na kushoto' (Nabhany 2012). Isitoshe, maana asilia ya *nyeti* ni '-enye umuhimu, -enye kuhitaji makini, -enye thamani'. *Suala ~* lakini katika Kiswahili cha kisasa 'nyeti' hutumiwa kitasfida kutajia *sehemu za siri za mwanadamu, uchi.* Amepigwa ***nyeti zikabaki nje.*** Hapa neno 'nyeti' limepata maana ya ziada. Fauka ya haya, maana ya awali ya 'tupu' ni – *siyo na kitu ndani, bila kuvaa chochote, uchi* (Burt 1910). Katika Kiswahili cha kisasa, neno *tupu* limepata maana ya ziada. Hutumiwa kama tasfida ya *kiungo cha binadamu; kuma, mboo na mkundu kinachotumiwa kunyea na kukojoa* (TUKI 2013). Maneno mengineyo yanayotumiwa kuwakilisha sehemu hizi ni *mbele, sehemu za siri* na *sehemu fiche*.

(ii) Tasfida za Matendo Yanayohusiana na Ngono
Katika kumbo hili maneno yafuatayo yamechanganuliwa:

(1) *Ngono, Baka, Uroda, Jamiiana, Saga, Shoga*
Maana ya awali ya *ngono*, ilikuwa 'usingizi'. Neno hili linatokana na kitenzi '*gona*' - kulala usingizi mnono (Krapf 1882).' Kitenzi hiki pia hupatikana katika lugha za Kibantu k.v. Kikamba, Kimeru, Kikuyu na Kiembu kwa maana hiihii. Katika Steere

(1870) ngono ni *zamu ya mke kulala na mumewe*. Krapf (ibid) anaeleza kuwa zamu ya suria inapofika ya kwenda chumbani mwa bwanake kumpa *ushirika wa kitanda*, ilisemekana kimafumbo kuwa *anampa ngono* (usingizi). Matumizi haya yalikuwa ya kitasfida. Katika Kiswahili cha Karne ya Ishirini na Moja, *ngono ni tendo la mwanamke na mwanamume kujamiiana*. 'Mgoni' ni mtu anayefumaniwa akizini. Maana ya neno imehama kutoka 'usingizi' hadi 'tendo la kujamiiana'. Pia, neno '*jamiiana*' ni tasfida yenye asili katika shina la Kiarabu [jamii] lenye maana ya 'kundi la watu'. Basi kujamiiana ni 'mwingiliano baina ya watu wa kundi fulani ili kuimarisha mahusiano' (socialization). Kitendo 'jamiiana' kinatumiwa kitasfida na mafumbo kupunguza aibu zinazoambatana na suala la ngono. Aidha, maana ya awali ya *uroda* ilikuwa *–enye raha, inayopendeza* (Massamba 2004) kabla ya kutumika kama tasfida ya ngono. Katika maana ya kisasa ya 'uroda' ni *tendo la kujamiiana* (TUKI 2013).

Iwapo ngono imeshurutishwa, tasfida zifuatazo kadhaa zimeibuka. Kwa mfano maana ya awali ya 'baka' ni *doa au alama iliyo juu ya kitu au mnyama, shika kitu kwa nguvu au ghafla, bamba.* Katika Krapf (1882), *bakata* ni tendo la 'kushika kitu kwa mikono na kukibebea mbele yako' Katika kisasa *(ku)baka* ni 'kushurutisha mtu kufanya ngono bila ridhaa yake'. Hutumiwa kitasfida kama njia ya kufunika aibu zinazoambatanishwa na tukio la kunajisiwa· *Kunajisi* pia ni tasfida ambayo maana yake asilia ni *tia uchafu, dhambi;* maneno yanayopunguza makali ya dhana husika. Ni mwiko kueleza tukio hili kinagaubaga hasa mbele ya watoto. Kwa maoni ya mwandishi, maneno 'baka' na 'najisi' yametwikwa hisia kali na wakereketwa wa haki za binadamu kiasi kwamba yanaibua hisia zenye aibu kwa kiasi fulani. Huenda tasfida nyingine zikazuka kukabili hali hii.

Fauka ya hayo, kitenzi 'saga' kilikuwa na maana ya ku-pondaponda kitu hadi kiwe mfano wa ungaunga, sababisha kitu kiishe polepole kwa kukisugua na kingine (Krapf 1882). Awali Waswahili walisaga nafaka kwa *mawe ya kusagia*. Jiwe kubwa la chini liliitwa *mama* na dogo la juu likiitwa *mwana* (Johnson 1939). Katika mwisho wa Karne ya Ishirini, kitenzi –saga kilianza kutumika kama tasfida ya 'kitendo cha kufanya ngono kati ya wanawake wawili kwa kugusanisha tupu zao' (TUKI 2013). Msagaji basi ni mwanamke anayejamiiana na mwanamke mwingine.

Aidha, *shoga* ni neno lenye asili ya Kiunguja lenye maana ya *rafiki wa kike wa mwanamke; bui* (Kiamu), *haviya* (Kitukuu). Neno asilia lilitumiwa baina ya watu wa jinsia ya kike pekee na pili, maana asilia ilikuwa chanya lakini sasa imekuwa hasi na yenye aibu. Inayoeleweka hapa ni kuwa mwanzoni, matumizi ya 'shoga' kwa wanaume yalikuwa ya kitasfida ili kufunika tabia iliyokatazwa katika jamii ya Waswahili. Baada ya matumizi yake kuzoeleka nayo dhana husika 'iliambukizwa' hisia hasi na hatimaye kudhalilika. Maana iliyosambaa zaidi katika Karne ya Ishirini na Moja ni, *mtu mwanamume anayejamiiana na mwanamume mwingine* labda kutokana na mabadiliko ya kitamaduni, athari za utandawazi na mwamko wa watetezi za haki za mashoga kuanzia mwishoni wa Karne ya Ishirini. Kuna baadhi ya nchi duniani zilizohalalisha ndoa kati ya 'mashoga'. Ni dhahiri neno lenyewe limepata mashiko au nguvu zaidi kuliko neno asilia.

Tasfida nyingine za karibuni ni *mpango wa kando* na *sponsa* (utohozi wa *sponsor)* zilizowakilisha dhana mbalimbali za mapenzi haramu. 'Mpango wa kando' huwakilisha mke au mume wa pembeni aliyewekwa na mtu aliye katika ndoa. Usponsa ni uhusiano wa kimapenzi ambapo mhusika aghalabu aliye tajiri na mkubwa kiumri humfadhili mwenzake kifedha ili naye amlipe kimapenzi. Uhusiano wa aina hii huwa kinyume na kaida, maadili na matarajio ya jamii. Matumizi ya maneno haya bila shaka yamezalisha maana ya ziada kwa maneno husika.

(iii) Tasfida Zinohusiana na Ujauzito
Katika kumbo hili maneno yafuatayo yamechanganuliwa:

(2) *Mjamzito, Mji, -fungua, pokea*

Neno *mjamzito* ni nomino ambatani iliyounganisha shina la kale, *mja*[2] (binadamu) na *–zito* yenye maana ya nje 'binadamu aliye mzito'. Neno hili hutumiwa kama tasfida ya *mwanamke aliye na mimba* (TUKI 2013). Nayo maana asili ya neno *mji* ilikuwa 'ukoo au kabila'. Kwa Waswahili, *wanamji* walikuwa watu wa nasaba moja waliokuwa chini ya utawala wa mzee (Abdulaziz 1979). Maana ya ziada ya mji ni *mahali panapoishi watu wengi na penye shughuli mbalimbali, mwandani katika kaburi.* Hatimaye mji hutumiwa kama tasfida ya *mfuko ambamo mtoto hukaa tumboni mwa mamake.* Desturi ya Mwafrika ilikuwa kufumba maswala yanayohusiana na mimba. Kadhalika, kitenzi *kujifungua* kinawakilisha kitasfida *tendo la kuzaa.* Vilevile, *mpokezi* hutumiwa kama tasfida ya neno *mkunga* (Nabhany 2012).

(iv) Tasfida za Vitu Vitokavyo Mwilini na Vitendo Vyake
Katika kumbo hili maneno yafuatayo yamechanganuliwa:

(3) *Choo, Msalani, Haja, -nya, Kinyesi, -endesha, -saidia, Mwezi*

Maana msingi ya *choo* (*kiolo* katika Kikale) ni 'chumba cha kuogea au cha kwenda kuendea haja kubwa au ndogo, msalani'. Waswahili na wenyeji wengine wa Afrika Mashariki huona aibu kutaja vimtokavyo mtu anapoenda chooni. Kwa Waswahili walitumia tasfida *choo* (chumba) na metonimu ya dhana finyu ya mavi. Kwa hivyo maana ikahama kutoka *chumba* hadi kwa *kinyesi.*

Nayo maana asilia ya neno *msala* ilikuwa *mkeka wa duara au zulia ndogo ya kuswalia* kama ilivyobainika katika Burt (1910). Katika Kiswahili cha Karne ya Ishirini na Moja, *msalani* (ni - kielezi cha mahali) ni *mahali pa usafi, chumba maalum ambapo watu huenda haja, chooni. Ameenda ~.* Hapa 'mkeka wa kuswalia' ni tasfida ya 'kwenda chooni'.

Kuna maneno mengine yanayohusiana na dhana ya 'choo' ambayo yamebadilika kitasfida. Mfano mzuri ni neno *haja* lenye maana msingi 'mahitaji ambayo mtu anataka yatimizwe au apate, matakwa'. Haja yenyewe inaweza kuwa ya kimwili, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Neno hili lilipata maana mpya na kuwa tasfida *kwenda chooni.* Kuna *haja kubwa* (mavi) na *haja ndogo* (mkojo). Katika Kiswahili cha kisasa, mzungumzaji akisema kuwa angependa 'kwenda haja' bila shaka

---

[2] Katika Karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20, neno *mja* ilikuwa tasfida ya *mtumwa* (Taz. Krapf 1882: 229, Burt 1910:202).

wasikilizaji wanaelewa wazi anasumbuliwa na mkojo au mavi, jambo ambalo ni mwiko kusema kinagaubaga.

Maana asilia ya *(ku)nya* ni *kitendo cha kutoa kitu kiowevu au cha majimaji*. Steere (1870) na Burt (1910) walisema kuwa ku-**nya** ni 'kuanguka kwa kitu kama vile mvua' kwa mfano katika: *Mvua yanya* yaani 'Mvua inanyesha'. A*isifuye mvua imemnyea*. Kauli 'nya mayai' ilitumiwa kumaanisha 'atama au taga mayai' (Steere ibid). Katika Kiswahili cha kisasa, neno 'ku-nya' hutumiwa kama tasfida ya *tendo la kwenda haja kubwa*. Maana hii badiliko ndiyo imeorodheshwa ikiwa ya kwanza katika kamusi ya TUKI (2013). Inaonekana tasfida hii pia imedhalilika baada ya matumizi ya muda mrefu na maneno mengine kubuniwa.

Kinachomtoka mtu kimepewa jina *kinyesi*. Maana awali ya kinyesi ilikuwa 'hali ya kuona vibaya kwa sababu ya uchafu au kuchukizwa na kitu ona kinyaa' (Burt 1910). Basi kinyesi, kinyaa na kinyezi ni maneno ya wanda moja licha ya tofauti ndogo za kifonolojia. Kinyezi humaanisha 'kuona vibaya kwa sababu ya uchafu'. Kwa kuwa mavi ni uchafu unaosababisha watu kuona kinyaa, basi neno 'kinyesi' likabanwa kutajia mavi. Huu ni *ufinyizi wa maana*. Linatumika kitasfida kupunguza hisia chukizi kwa wanajamii. Hata hivyo, utafiti ulibainisha kuwa matumizi yake ya muda marefu yamesababisha neno hili pia kupata hisia za aibu.

Kadhalika, kitenzi *–ji-saidia* kinachomaanisha *–pa* au kuwezesha mtu kupata mahitaji yake. Kiambishi {ji} kinachowakilisha dhana ya mtu kujitendea jambo mwenyewe. Awali maana ilikuwa chanya lakini tangu itumike kama *tasfida* ya 'enda choo' pia imedhalilika kimaana. Katika Kiswahili cha Karne ya 21, mhusika akisemekana 'ameenda kujisaidia' inaeleweka bayana kuwa 'ameenda msalani'. Fauka ya hayo, kitenzi *endesha* chenye maana msingi ya 'kitendo cha kuongoza chombo cha usafiri kama gari, baiskeli na kadhalika kuelekea mahali fulani' katika kisasa hutumiwa kikiwa tasfida ya dhana yenye aibu ya 'kuhara'. Inaonekana tendo lenyewe limepigwa chuku.

Maana ya awali ya *mwezi* ilikuwa 'gimba mojawapo linalozunguka dunia mara moja kila siku 28 na linang'ara usiku'. Polome (1967) anasema neno *mwezi* lilitokana neno **[mogɛdi]* lenye mzizi *{gɛd} wa mame-bantu lenye maana ya 'waka, toa mwangaza'. Fonimu /d/ ilibadilika na kuwa /z/ kuunda [mwɛzi]. Inasadifu kuwa mwanamke hupata damu ya hedhi baada ya siku ishirini na nane na kwa hivyo neno 'mwezi' likawa *tasfida* ya kipindi hicho cha hedhi. Wakati mwingine neno *damu,* ufupisho wa 'damu ya hedhi' na neno 'mgeni' hutumiwa kitasfida kuwakilisha dhana husika. Kauli: *Fatuma ana damu/mgeni leo* ina maana inayoeleweka wazi na wanajamii. Wanajamii huelewa maana ya 'damu' kutegemea muktadha na wahusika. Maana hujikita katika utamaduni na tajriba za pamoja za wanajamii.

(v). Tasfida Zinazohusiana na Mahusiano

Kuna baadhi ya maneno yanayoambatana na mahusiano ambayo yamebadilika kitasfida. Tutachanganua mifano ifuatayo:

(4) *Dada, Bibi*

Maana asilia ya *dada* ni *ndugu mkubwa wa kike; kwa baba au mama*, *yaye* katika Kitukuu (Nabhany 2012). Katika Kiswahili cha kisasa huwakilisha *ndugu <u>mkubwa</u> wa kike*[3], *ndugu yeyote wa kike, jina la heshima analoitwa mwanamke yeyote na wanavyoitwa waumini wa kike kanisani.* Hata hivyo, *kidada* (udogo au udunishaji) hutumika pwani ya Kenya kama tasfida ya *mwanamke aliye kahaba, kimada, hawara au malaya.* Nalo neno *bibi* ni *mwanamke mzaa mama au baba katika Kiamu na Kiunguja.* Asili ilikuwa Kihindi (TUKI, 2013). Pia, lina maana '*mke wa*' k.v. ~ *wa Hassan.* Katika kisasa linatumiwa kama 'jina la heshima la mwanamke yeyote' na kama tasfida ya *mwanamke hawara, kimada* (TUKI: ibid).

(vi) Tasfida za Vitu Vilivyoharamishwa na Jamii au Serikali

Katika kumbo hili mifano ifuatayo imechanganuliwa:

(5) Unga, Mtindi, Chai, Maji

Maana awali ya *unga* ilikuwa "nafaka iliyosagwa ikawa mfano wa vumbi. Neno hili lilianza kutumika katika Kiswahili miaka ya 1908-1909 wakati tajiri aliyeitwa Bill Spencer alianzisha kiwanda cha kusaga nafaka katika sehemu za Turbo, kaunti ya sasa ya Uasin Gishu. Kiwanda kilichojulikana kama Uasin Gishu Growers Assosiation, kwa ufupi UNGA. Kiwanda kilitumia mitambo iliyoendeshwa kwa maji yaani 'turbines,' kutoka Mto Sosiani kusagia mahindi na kusambaza pakiti za kilo mbili mbili zilizokuwa na maadishi U.N.G.A. Wenyeji walishindwa kutamka neno *turbine*, wakaunda jina Turbo. Mnamo mwaka wa 1919, Midan aliyekuwa akihariri *Kamusi ya Kisuaheli* iliyokuwa imetungwa na Krapf aliliingiza neno 'unga' rasmi katika maandishi ya Kiswahili. Kuanzia wakati huo 'kitu chochote kilichosagwa na kuwa kama vumbivumbi' kiliitwa unga. Katika Kiswahili cha kisasa neno 'unga' hutumiwa kama sitiari ya *riziki*. Nahau *tafuta* ~. Aidha, neno hili hutumiwa kama tasfida ya dawa za kulevya aina ya 'heroine· Heroine safi huwa mfano wa unga mweupe. Baadhi ya misimu inayowakilisha heroine ni *kichuri, kiketi, mizigo, poni, popy, junk, horse na maponari*. Majina haya hutumiwa kimafumbo baina ya waraibu ili kuepa mkono mrefu wa sheria. Misimu kama hii hubadilikabadilika kila kuchao.

Maana awali ya *mtindi* ilikuwa 'maziwa yaliyoganda na kupata ukali' (Krapf 1882). Pia maziwa yanayobaki baada ya kutolewa siagi. Katika kisasa, neno husika hutumika kama tasfida ya pombe kwa nia ya kuepa hisia zisizofaa zinazohusishwa na pombe hasa ile haramu. Kuna nahau maarufu *piga mtindi* inayomaanisha *kunywa pombe*.

Maana msingi ya 'chai' ni majani ya mchai, kinywaji kilichotengenezwa kwa majani ya mchai. Neno hili lina asili ya Kihindi. Hutumiwa ikiwa tasfida ya *rushwa, mrungura, chauchau au hongo*. Tasfida nyingine mashuhuri ni *mvugulio,* kutokana na kitenzi *vugua:* 'tokeza upande wa pili wa kitu baada ya kupitia katikati k.v. msitu' (TUKI 2013). Pia *kitu kidogo*. Maneno hayo hutumiwa kufunika maovu husika. Pia, neno 'maji', *kiowevu kinachopatikana kutokana na mvua, mito, bahari,*

---

[3] Ndugu mdogo wa kike huitwa mnuna. Kwa wazungumzaji wengi wa Kiswahili dada na mnuna huwakilishwa na neno 'dada'.

maziwa na visima katika kisasa hutumiwa kama tasfida ya *pombe*. Pia hutumiwa kuwakilisha dhana ya *'wizi wa mitihani'*. *Tulipata ~ kabla ya mtihani huo.*

(vii) Tasfida za Kifo

Katika kumbo hili mifano ifuatayo imechanganuliwa:

(6) *Aga, Punga mkono, Enda zake, Acha, Hayati, Fariki, Buriani*

Jamii nyingi za Kiafrika hadi leo hii hutumia neno 'kifo' kwa uangalifu na pengine kama neno-mwiko. Dhana ya kifo inawakilishwa kimafumbo na maneno mengineyo. Mathalani, maana ya kimsingi na ya awali kitenzi *–aga* ilikuwa *omba ruhusu ya kuondoka* (Burt 1910). Ilikuwa desturi na heshima kwa Waswahili kuagana na mtu mwenzake kabla ya kuondoka na kumwarifu mngeonana baadaye. Katika mpito wa wakati, dhana ya kuaga ilianza kutumika kitasfida kuwakilisha dhana ya *kifo* kama inavyodhihirika katika kamusi ya EAEP (2011). Leksia yenyewe inatoa taswira ya hali ambapo aliyeondoka atarejea tena hivyo kupunguza makali na hisia za kupoteza mpendwa wako milele. Tasfida nyingine za kifo ni pamoja na *punga mkono* (toa ishara kwa kupepea mkono kuashiria umeondoka kwa muda), *-endazake* (-enda mahali kusikojulikana) na *–acha* (ondoka) na *kata roho* (nahau inayomaanisha kufa). Pia kuna maneno mengine ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu kama vile *hayati* (Yu hai/ uhai, harakati za viungo vya mwili wa kiumbe katika hali ya kufanya kazi na kukua; muda wa mtu baina ya kuzaliwa mpaka kufikia kufa, kinyume cha mauti." (Hussein 2016). Katika kisasa hutumiwa kitasfida kuwakilisha "mtu ambaye amefariki, marehemu" (TUKI 2013). Awali ilihusishwa na *uhai* lakini kwa sasa hutumika kwa *wafu*. Hutumiwa kama jina au kitangulizi cha marehemu aliyekuwa maarufu k.m. ~ Mzee Jomo Kenyatta na *-fariki* (kuwa mbali na, -tengwa). Tasfida zingine ni *-ipa dunia buriani*, *-ipa dunia kisogo* na *-enda jongomeo zinazotoa matumaini fulani ya marehemu kurejea tena au* katika *Al Inkishafi*, ubeti 24, neno la kale *manaya* ndilo lililotumiwa kuwakilisha *kifo au mauti*. *Kiimba* ni neno la kale la maiti na lingali linatumiwa katika lugha kadhaa za Kibantu.

Uchanganuzi unabainisha kwamba maneno asilia yanapodhalilika kimaana na kuwa miiko, kuna mazoea ya kutumia maneno mageni kuziba pengo husika. Kuna uwezekano mkubwa kwamba matumizi ya neno *damu* (mkopo kutoka Kiarabu) katika nafasi ya neno la Kiswahili *ngeu* (ng'eu) ilikuwa juhudi za kukwepa hisia mbaya zilizoambatana na neno *ngeu* au *mweni*. Katika jamii nyingi za Kiafrika hadi leo hii, dhana ya '*damu*' inahusishwa na *kifo* au *vita*. Mkondo huu labda ndio ulichukuliwa na neno la mkopo *fariki* kuwakilisha dhana ya *kufa* na *hayati* kuwakilisha *mfu*. Ni dhahiri kuwa kuingia kwake katika Kiswahili kulitokana na sababu za kitasfida na si kwa sababu ya ukosefu wa msamiati mwafaka. Inaonekana kuwa maneno yanapobadilika na kuambatanishwa na 'hisia mbaya' au kuwa maneno-mwiko husababisha maneno mengine kutwikwa jukumu la kuwasilisha maana husika. Maneno mpya yanaweza kubuniwa au kukopwa ili kupunguza umatusi umatusi wa neno lililoathiriwa.

Hitimisho

Makala haya yamejadili nafasi ya tasfida na miiko katika mabadiliko ya maana za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa kulinganisha mifano ya maneno mahususi ya Kiswahili cha kabla ya Karne ya Ishirini na Kiswahili cha Karne ya Ishirini na Moja. Uchanganuzi umeonyesha bayana kuwa tasfida na miiko imechangia pakubwa kuleta mabadiliko ya maana za maneno ya Kiswahili. Imebainika kuwa mwanadamu hujaribu awezavyo kuepuka maneno-mwiko anapotumia lugha. Hapendi fedheha, aibu au kuvunja kaida zilizopo za matumizi ya lugha katika jamii. Tasfida ni mbinu ya kutosheleza hitaji hili. Yeye huchukua maneno yaliyopo katika lugha na kuyatwika majukumu mapya kwa nia ya kusitiri aibu husika; jambo ambalo husababisha mabadiliko ya maana za maneno husika. Imebainika kuwa neno likitumika kitasfida kwa muda mrefu mara nyingi 'huambukizwa' hisia hasi na hatimaye kudhoofika na kuwa neno-mwiko. Mbinu mbili kuu za mabadiliko ya kisemantiki zinazoambatanishwa na tasfida na miiko ni *udhoofikaji* na *uimarikaji wa maana*. Mwanadamu ana uwezo thabiti wa kudhibiti miiko kwa kuhamisha dhana kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine kwa nia ya kudumisha heshima na kuhifadhi utamaduni wa jamii. Yamkini maana huwa na sifa ya kitamaduni.

Marejeleo

Abdulaziz M. H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Allan, K., & Burridge, K. (1991). *Euphemism and Dysphemism.* Oxford: Oxford University Press.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Burt, F. (1910). *Swahili Grammar and Vocabulary.* London. Society for Promoting Christian Knowledge Northumberland Avenue, W.C.

E. A. E. P. (2011). *Comprehensive Swahili – English Dictionary.* Nairobi: E.A.E.P. Limited.

Fromkin, Rodman na Hyams (2011). *An Introduction to Language and Linguistics*, 9th edition. USA: Wadsworth Cengage learning.

Gachara, M. (2012). Metaphors of Gikuyu Marriage Negotiations: A Cognitive Linguitics Perspective. Ph. D Thesis. Kenyatta University (Unpublished).

Gathiga, M. G. (2010). A Cognitive Linguistics Analysis of Gikuyu Euphemism. M.A. Thesis. Kenyatta University (Unpublished).

Gichuru, T. M (2020). "Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Ulinganisho wa Kikale na Kisasa". Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Hussein, A. H. (2016). "Mabadiliko ya Kifonolojia na Kisemantiki katika Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu". Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Haijachapishwa).

Johnson, F. (1939). *A Standard Swahili-English Dictionary.* Oxford: Oxford University Press.

Kineene wa Mutiso (2005). *Utenzi wa Hamziya.* Dar es Salaam: TUKI

Krapf, J. L. (1882). *Dictionary of Suaheli Language.* London: Trubner and Co. Ludgate Hill.

Lakoff, G. & Mark, J. (1980). *Metaphor we live by.* Chicago: Chicago University Press.

Massamba, D. P. B. (Mh.) 2004. *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Nabhany, S. A. (2012). *Kandi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Aera Kiswahili Researched Products.

Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook.* Washington: Centre for Applied Linguistics.

Samoškaite, L. (2011). 21st Century Euphemism in English Newspapers: Semantic and Structural Study. MA paper, *Vilnius pedagogical university*. Gs.elaba.it/elaba: 2084534pdf

Schadeberg, T. C. (1991). 'Historical Inferences from Etymologies' in *Stanslaw Pilasze- Wicz & Eugenius*. Pdf document

Steere, E. (1870). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar. Revised Edition* by *Madan (1919)*, London: Society for Promotion of Christian Knowledge.

TUKI (2004, 2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.